8. Undwaji wa kamati.
9. Uteuzi wa Msajili.
10. Majukumu ya Msajili.
11. Sekretarieti ya Baraza.
12. Malipo ya wajumbe wa Baraza.

SEHEMU YA TATU  
USAJILI, UANDIKISHWAJI NA UORODHESHAJI WA  
WAKEMIA, MAFUNDISANIFU KEMIA NA MAFUNDI  
SANIFU KEMIA WASAIDIZI

13. Sifa za kusajiliwa, kuandikishwa na kuorodheshwa.
14. Mafunzo kwa vitendo.
15. Usajili wa muda.
16. Utoaji wa cheti.
17. Rejesta, Orodha na Listi.
18. Usitishaji, ubatilishaji au ufutaji wa cheti.
19. Urejeshaji wa majina katika Rejesta, Orodha au Listi.

20. Zuo la matumizi ya cheo.

SEHEMU YA NNE  
MASHARTI YA FEDHA

21. Vyanzo vya mapato.
22. Taarifa za fedha za mwaka.
23. Uwasilishwaji wa taarifa ya fedha ya mwaka.
24. Usimamizi na udhibiti wa fedha.
25. Bajeti ya mwaka na bajeti ya nyongeza.
26. Misingi ya uendeshaji.
27. Mamlaka ya kuwekeza.

SEHEMU YA TANO  
MASHARTI YANAYOHUSU NIDHAMU

28. Upokeaji wa malalamiko kwa Msajili.
29. Kusimamishwa kwa muda kupisha uchunguzi.
30. Taratibu za uchunguzi.
31. Mamlaka ya nidhamu ya Baraza.
32. Mamlaka ya kumwita shahidi.
33. Kushindwa kuhudhuria uchunguzi.
34. Rufaa.

SEHEMU YA SITA  
MASHARTI JUMLA

35. Kanuni.
36. Taratibu.
37. Makosa na adhabu.
  
38. Kutangaza majina ya wanataaluma wa kemia.
39. Kinga kwa makosa.
40. Ufililishaji wa makosa.

---

JEDWALI

---

**TAARIFA**

Muswada huu utakaowasilishwa Bungeni umechapishwa pamoja na madhumuni na sababu zake kwa ajili taarifa ya jumla kwa umma.

Dar es Salaam,  
17 Mei, 2016

**JOHN W. H. KIJAZI**  
*Katibu wa Baraza la Mawaziri*

**MUSWADA**

*wa*

**Sheria ya kuanzishwa Baraza la Wanataaluma ya Kemia, kuweka mamlaka, majukumu, usimamizi na udhibiti wa Wanataaluma ya Kemia; na kuweka masuala mengine yanayohusiana nayo.**

**IMETUNGWA** na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**SEHEMU YA KWANZA  
MASHARTI YA UTANGULIZI**

Jina na Tarehe  
ya kuanza kutumika

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Usimamizi wa Wanataaluma wa Kemia, 2016 na itaanza kutumika katika tarehe ambayo Waziri atatangaza kwenye Gazeti la Serikali.

Matumizi

**2.** Sheria hii itatumika Tanzania Bara.

Tafsiri

**3.** Katika Sheria hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-  
“cheti” maana yake ni cheti kilichotolewa chi-

ni ya kifungu cha 17;

“kamati” maana yake ni kamati yoyote iliyoundwa chini ya kifungu cha 8;

“Baraza” maana yake ni Baraza la Wana taaluma wa Kemia lililoanzishwa chini ya kifungu cha 4;

“mwaka wa fedha” maana yake ni mwaka wa fedha wa Serikali;

“fundi sanifu kemia msaidizi” maana yake ni mtu mwenye cheti cha kemia au fani katika kemia kutoka katika taasisi inayotambuliwa;

“cheti” maana yake ni cheti kinachotolewa chini ya kifungu cha 16;

“mkemia” maana yake ni mtu aliyetunukiwa shahada ya kemia au fani nyingine katika kemia kutoka katika taasisi inayotambuliwa;

“fundi sanifu kemia” maana yake ni mtu ambaye ametunukiwa stahada ya kemia au fani nyingine katika kemia kutoka katika taasisi inayotambuliwa;

“mwana taaluma wa kemia” maana yake ni mkemia, fundi sanifu kemia na fundi sanifu kemia msaidizi aliyesajiliwa, orodheshwa au kuwekwe kwenye listi kwa maana hiyo;

I “Waziri” maana yake ni Waziri anayehusika na masuala ya afya;

“mwanataaluma” maana yake ni mkemia, fundi sanifu kemia au fundi sanifu kemia msaidizi aliyesajiliwa, orodheshwa au kuandikishwa kwa mujibu wa Sheria hii;

“Rejesta” itamaanisha rejesta iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 19;

“Msajili” maana yake ni Msajili wa Baraza aliyeteuliwa chini ya kifungu 9; na

“mamlaka ya usimamizi” maana yake ni mamlaka yoyote iliyopo kisheria ambayo inatumika kama mwajiri wa wana taaluma wa kemia.

“Orodha” maana yake ni Orodha ya mafundi



sanifu kemia iliyoanzishwa katika kifungu cha 17;

“List” maana yake ni Listi ya mafundi sanifu kemia wasaidizi iliyoanzishwa katika kifungu cha 17.

SEHEMU YA PILI  
BARAZA LA WANATAALUMA WA KEMIA  
NA FUNDI SANIFU KEMIA

Kuanzishwa na  
muundo wa  
Baraza

4.-(1) Linaanzishwa Baraza litakalojulikana kama Baraza la Wanataaluma wa Kemia.

(2) Baraza litakuwa ni chombo kinachotambulika kisheria na litakuwa ni chombo endelevu na cha kudumu na kitakuwa na lakiri yake rasmi.

(3) Kwa kutumia jina lake, Baraza litakuwa na uwezo wa-

- (a) kushtaki na kushtakuwa;
- (b) kununua na kumiliki mali yoyote inayohamishika na isiyohamishika;
- (c) kukopa na kukopesha;
- (d) kuingia mikataba au kufanya mi-amala yoyote ile; na
- (e) kufanya jambo au kitu chochote ambacho chombo chochote chenye hadhi ya kisheria kinaweza kufanya.

(4) Bila kujali masharti yaliyotangulia katika kifungu hiki, Mwanasheria Mkuu wa Serikali atakuwa na haki ya kuingilia kati kati-ka kesi au shauri lolote lililofunguliwa dhidi ya Baraza.

(5) Pale ambapo Mwanasheria Mkuu wa Serikali anaingilia kati katika shauri lolote kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2), basi masharti ya Sheria ya Mwenendo wa Mashauri dhidi ya Serikali, yatatumika.

(6) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (4), Baraza itakuwa na jukumu la kumtaarifu Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu shauri lolote lililofunguliwa au linalokusudiwa

kufunguliwa dhidi ya Baraza.

(7) Baraza litakuwa na Wajumbe tisa watakaoteuliwa na Waziri kama ifuatavyo-

- (a) Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Waziri;
- (b) mwakilishi wa Mkemia Mkuu wa Serikali;
- (c) mwakilishi wa chama cha wana-taaluma wa kemia Tanzania;
- (d) mkemia mmoja mwenye cheo cha uandamizi au zaidi anayewakilisha vyuo vikuu vya umma;
- (e) mkemia mmoja mwenye cheo cha uandamizi au zaidi anayewakilisha vyuo vikuu binafsi;
- (f) Afisa Sheria atakayependekezwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali;
- (g) fundi sanifu kemia au fundi sanifu kemia msaidizi;
- (h) Afisa wa cheo cha uandamizi au zaidi kutoka Utumishi; na
- (i) askari polisi wa cheo cha Inspekta au zaidi anayemwakilisha Inspekta Generali wa Polisi.

(8) Utaratibu kuhusu muda wa wajumbe wa Baraza, taratibu za shughuli za Baraza na mambo mengine kuhusiana na Baraza yatakuwa kama yanavyoonekana katika Jedwali la Sheria hii.

(9) Waziri anaweza, kwa amri itakayochapishwa kwenye gazeti la Serikali, kufanya marekebisho kwenye Jedwali la Sheria hii.

Majukumu ya Baraza

**5.-(1)** Baraza litakuwa na wajibu wa-

- (a) kuwasajili, kuwaorodhesha na kuwaandikisha wanateknolojia na wanateknolojia wasaidizi wa kemia.

- (b) kuweka viwango, kutunga kanuni za maadili na kudhibiti mwenendo wa wanataaluma ya kemia.

(2) Bila kuathiri masharti ya ujumla kifungu kidogo cha (1), Baraza litatekeleza

yafuatayo-

- (a) kumshauri Waziri kuhusu masuala yanayohusu wanataaluma ya kemia;
- (b) kuchunguza malalamiko yoyote dhidi ya mwanataaluma ya kemia;
- (c) kusimamia na kuendeleza maadili ya taaluma ya kemia;
- (d) kuendeleza ushirikiano baina ya Baraza na taasisi nyingine au mashirika mengine yanayojihusisha na taaluma ya kemia;
- (e) kusimamia hesabu na mali za Baraza au mali nyingine zozote zilizokabidhiwa kwa manufaa ya Baraza;
- (f) kuweka viwango vya tozo zitakazolipwa kwa Baraza kwa ajili ya huduma zitakazotolewa na Baraza;
- (g) kushughulikia masuala yanayoathiri taaluma ya kemia, na kuchukua hatua stahiki kama ambavyo Baraza litaona inafaa;
- (h) kutoa, kuhuisha, kurudisha na kufuta kibali cha kufanya kazi za mwanataaluma ya kemia; na
- (i) kutekeleza majukumu mengine ambayo Waziri ataelekeza; na

Mamlaka ya Baraza

**6.-(1)** Baraza litakuwa na mamlaka yafuatayo-

- (a) kuainisha sifa za mwanataaluma ya kemia atakayesajiliwa, kuorodheshwa au kuandikishwa;
- (b) kukasimisha mamlaka na majukumu yake kwa mtu yeyote wa taaluma aliyesajiliwa chini ya Sheria hii na kwa kipindi kama itakavyoonekana inafaa, isipokuwa hatakasimu mamlaka ya
  - (i) nidhamu;
  - (ii) kupitisha bajeti ya mwaka, bajeti ya nyongeza, taarifa

- ya hali ya fedha na taarifa nyingine za kiuhasibu; na
- (iii) kukopa kwa niaba ya Baraza.
- (c) kuondoa au kurejesha jina kwenye rejesta au orodha kutegemeana na masharti ambayo Baraza litaweka;
- (d) kuteua wakaguzi watakaofanya ukaguzi au kazi yoyote kwa niaba ya Baraza;
- (e) kudai taarifa kutoka kwa mtu aliyesajiliwa, kuorodheshwa au kuandikishwa au kujihusisha na shughuli za kikemia pale itakapoonekana inafaa;
- (f) kuchunguza suala lolote, lalamiko, shitaka au tuhuma za kukiuka maadili dhidi ya mtu aliyesajiliwa, kuorodheshwa au kuandikishwa;
- (g) kupitisha bajeti ya mwaka ya Baraza; na
- (h) kuruhusu vyuo vya mafunzo kwa wanataaluma wa kemia.

Wajumbe wa Baraza na Kamati

**7.** Mtu hatateuliwa kuwa mjumbe wa Baraza au Kamati isipokuwa tu kama mtu huyo ni Mtanzania aliyesajiliwa, kuorodheshwa au kusajiliwa kama mwanataaluma wa kemia.

Uundwaji wa kamati

**8.-(1)** Baraza linaweza kwa madhumuni ya kuhakikisha ufanisi katika kutekeleza majukumu yake na kwa mamlaka, kuanzisha kamati mbalimbali kufanya kazi zake, kama itakavyoelekezwa.

(2) Bila kuathiri masharti ya jumla ya kifungu kidogo cha (1), Baraza litaunda kamati zitakazohusika na masuala yafuatayo-

- (a) usajili, uorodhesha na uandikishaji;
- (b) maadili na nidhamu; na
- (c) mapitio ya utendaji na maendeleo ya taaluma.
- (3) Majukumu, muundo na mienendo

ya kamati yatatajwa katika kanuni zitakazotengenezwa chini ya Sheria hii.

(4) Kamati inaweza kumualika mtu yeyote kusaidia Kamati kuhusu suala lolote kadri itakavyoona inafaa.

Uteuzi wa Msajili

**9.**-(1) Waziri atamteu mkemia mkuu au mkemia mwandamizi mwenye shahada ya uzamili kutoka kwenye utumishi wa umma kuwa Msajili wa Baraza.

(2) Msajili atakuwa katibu wa Baraza.

(3) Msajili atakuwa madarakani, isipokuwa kama ajira yake itatenguliwa, kwa kipindi cha miaka mitatu na atakuwa na fursa ya kuteuliwa tena kwa kipindi kimoja kingine cha miaka mitatu.

Majukumu ya Msajili

**10.**-(1) Baada ya kupata idhini ya Baraza, Msajili-

(a) atawezesha kuchapishwa katika *Gazeti* la Serikali, mara baada ya kusajili, taarifa zilizoingizwa kwenye rejesta au orodha kuhusi-ana na kila mtu, na kwa maelekezo ya Baraza, mabadiliko au kufutwa kwa taarifa zilizomo;

(b) atatoa vyeti baada ya usajili, uoredheshwaji na uandikishwaji wa wanataaluma pamoja na kulipa tozo stahiki;

(c) Bila kuathiri masharti ya jumla ya kifungu kidogo cha (1), Msajili-

(d) atatunza taarifa za akaunti na kumbukumbu nyinginezo zinazohusu fedha na rasilimali za Baraza;

(e) atafungua akaunti moja au zaidi katika benki yoyote ya Biashara inayoaminika ili fedha zote zinazopokelewa kwa Baraza ziweze kuhifadhiwa;

(f) atandaa na kuzingatia makadario ya mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka;

- (g) atatekeleza maamuzi ya Baraza;
- (h) atandaa na kutangaza ripoti ya mwaka ambayo itajumuisha-
  - (i) akaunti ya uendeshaji ya Baraza kwa mwaka uliotajwa kwenye ripoti;
  - (ii) hesabu zilizokaguliwa; na
  - (iii) masuala mengine yataka-yoainishwa; na
- (i) atatekeleza majukumu mengine ambayo yanahitajika chini ya Sheria hii au yaliyoelekezwa na Baraza chini ya Sheria hii.

Sekretarieti ya Baraza

- 11.**-(1) Kutakuwa na Sekretarieti ya Baraza ambayo itajumuisha maafisa na watumishi wa Baraza-
- (a) Msajili; na
  - (b) Wafanyakazi wengine wataoteuliwa na Baraza.
- (2) Maafisa na watumishi wa Baraza watakuwa watumishi wa Serikali.

Malipo ya wajumbe wa Baraza

- 12.** Wajumbe wa Baraza na Sekretarieti watalipwa malipo kutoka katika mapato ya Baraza kama Waziri, baada ya kushauriana na Msajili wa Hazina, atakavyoomua.

## SEHEMU YA TATU

### USAJILI, UANDIKISHWAJI NA UORODHESHWAJI WA WAKEMIA, MAFUNDI SANIFU KEMIA NA MAFUNDI SANIFU KEMIA WASAIDIZI

Sifa za kusajiliwa, kuandikishwa na kuorodheshwa

- 13.**-(1) Mtu anayekusudia kusajiliwa, kuorodheshwa au kuandikishwa kama mkemia, fundi sanifu kemia au fundi sanifu kemia msaidizi, kwa mtiririko huo, atawasilisha maombi kwenye Baraza kwa mujibu wa utaratibu iliyoainishwa kwenye Jedwali la Pili la Sheria hii.
- (2) Mtu hataweza kusajiliwa, kuorodheshwa au kuandikishwa kama mwana-

taaluma wa kemia isipokuwa-

(a) kama mtu huyo anayo-

(i) shahada ya kemia au mchepuo wa kemia au fani yoyote inayohusiana na kemia kutoka katika taasisi inayotambulika;

(ii) stahada, endapo mwombaji ni fundi sanifu kemia; na

(iii) cheti, endapo mwombaji ni fundi sanifu kemia msaidizi;

(b) taaluma na mwenendo wake kwa ujumla vinamuwezesha kuwa na sifa za kusajiliwa kama mwanataaluma ya kemia.

(3) Waziri baada ya kushauriana na Baraza atatunga kanuni kwa ajili ya kuainisha vigezo vya ziada vitakavyotumika katika usajili, uorodheshaji na uandikishaji kadri litakavyoona inafaa.

Mafunzo kwa vitendo

**14.**-(1) Mkemia hatasajiliwa mpaka pale Baraza litakapojiridhisha kwamba amepitia mafunzo kwa vitendo kwa kipindi cha mwaka mmoja.

(2) Utaratibu na mahitaji ya mafunzo kwa vitendo yatakuwa kama yalivyoainishwa kwenye kanuni.

Usajili wa muda

**15.**-(1) Pale ambapo mtu ambaye si Mtanzania ataliridhisha Baraza kwamba-

(a) yupo au ana dhamira ya kuwepo Tanzania, kutokana na sifa za kuwa mwanataaluma ya kemia, kwa lengo la kufanya kazi maalumu au ambayo amekuwa akihusika nayo kwa kipindi kisichozidi miezi kumi na mbili;

(b) kabla ya kuingia Tanzania alikuwa anajishughulisha au akijishughulisha na taaluma ya kemia na anazo

sifa za kusajiliwa chini ya Sheria hii; na

- (c) taaluma na mwenendo wake kwa ujumla vinamwezesha kuwa na sifa za kusajiliwa,

anaweza akasajiliwa kwa muda.

(2) Baraza litahitaji mtu yeyote anayeomba kusajiliwa chini ya kifungu hiki kufika mbele ya kamati ya usajili na kuwasilisha nyaraka kuhusiana na kazi aliyopewa au ajira.

(3) Usajili wa mtu chini ya kifungu hiki utaendelea pale tu atakapokuwa anajihusisha na kazi maalumu aliyopewa na pale atakapocha kujihusisha au muda utakapoisha usajili wake utakoma.

(4) Usajili wa mtu chini ya kifungu hiki unaweza kuhuishwa kama baraza litakavyoona inafaa.

(5) Mtu yeyote atakayekwenda kin-yume na masharti ya kifungu hiki atakuwa anatenda kosa na atawajibika kulipa faini isiyopungua milioni tano au kifungu cha miaka miwili, au vyote kwa pamoja.

Utoaji wa cheti

**16.**-(1) Baraza litatoa cheti husika kwa aliyesajiliwa, kuorodheshwa au kuandikishwa na chini ya Sheria hii.

(2) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (1), cheti hicho kitakuwa na:

- (a) majina kamili na anwani ya mwombaji;  
(b) sifa za kitaaluma na cheo; na  
(c) masharti ambayo yanahusiana na cheti kinachoteuliwa.

Rejesta, Orodha na Listi

**17.**-(1) Kwa kuzingatia Sheria hii, Baraza litaanzisha, litaweka na kutunza Rejesta na Orodha ya Wanataaluma wa Kemia.

(2) Kila mtu aliyesajiliwa, kuandikishwa au kuorodheshwa, kabla ya tarehe 31 Desemba ya kila mwaka, atapeleka taarifa zake kwenye Baraza kwa namna ilivyoainishwa



kwa ajili ya jina lake kuendelea kuwemo kwenye Rejesta.

(3) Taarifa zilizowasilishwa katika kifungu kidogo cha (1), zitaambatana na tozo iliyoainishwa.

(4) Baraza linaweza kumuondoa mtu yeyote kutoka katika Rejesta, iwapo hafuati masharti ya vifungu vidogo (2) na (3).

(5) Mtu anaweza, baada ya malipo ya ada iliyoainishwa na katika kipindi kitakachoamuliwa, kukagua Rejesta, Orodha au Listi.

Usitishaji,  
ubatilishaji au  
ufutaji wa cheti

**18.**-(1) Baraza linaweza, kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii na baada ya kuridhika kwamba vigezo na masharti ya utoaji cheti vimekiukwa-

(a) kubatilisha, kusitisha au kufuta cheti kwa namna itakavyokuwa;

(b) kumtaarifu mtu ambaye cheti chake kimebatilishwa, kusitishwa au kufutwa; na

(c) kufuta jina la mtu ambaye cheti chake kimebatilishwa, sitishwa, au kufutwa kwa namna itakavyokuwa.

(2) Mtu ambaye jina lake limefutwa katika Rejesta, Orodha au Listi atapaswa, ndani ya siku thelathini tangu kufutwa, kuwasilisha katika Baraza cheti kilichotolewa chini ya kifungu cha 16.

(3) Mtu atakayeshindwa kuwasilisha cheti ndani ya kipindi kitakachowekwa atakuwa ametenda kosa.

Urejeshwaji wa  
majina katika  
Rejesta, Orodha  
au Listi

**19.**-(1) Pale ambapo jina la mkemia, fundi sanifu kemia au fundi sanifu kemia msaidizi limefutwa kutoka katika Rejesta, Orodha au Listi kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 18, jina la mtu huyo halitaingizwa tena katika Jedwali, Orodha au Listi ama kwa ada au bila ya ada.

(2) Pale ambapo amri imetolewa kwa ajili ya kufutwa kwa jina la mtu huyo kutoka katika Rejesta, Orodha au Listi, Baraza

linaweza, lenyewe au kwa maombi ya mhusika, na kwa namna yoyote ile, baada ya kufanya uchunguzi kama ambavyo Baraza litaona inafaa, litawezesha jina la mtu huyo kurudishwa katika Rejesta, Orodha na Listi, ama kwa ada au bila ya ada.

Zuio la matumizi ya cheo

**20.**-(1) Hakuna mtu, isipokuwa mwanaaaluma ya kemia wakati au baada ya kuanza kutumika kwa Sheria hii, atajifanya, atachukua, atajionesha, kwa namna yoyote ile kutumia cheo, nembo, au maelezo ambayo yataashiria kwamba ni mkemia, fundi sanifu kemia au fundi sanifu kemia msaidizi.

(2) Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na kifungu kidogo cha (1), atakuwa ametenda kosa na atawajibika kulipa faini isiyopungua milioni moja au kifungu kisichozi miaka miwili, au vyote kwa pamoja.

#### SEHEMU YA NNE MASHARTI YA FEDHA

Vyanzo vya mapato

**21.**-(1) Vyanzo vya mapato ya Baraza vitatokana na-

- (a) fedha zilizoidhinishwa na Bunge;
- (b) fedha zozote au rasilimali ambazo zinaweza kuwa zimebainishwa au kukusanywa kutoka vyanzo vingine;
- (c) mikopo iliyotolewa na Serikali au na mtu au chombo kingine chochote;
- (d) tozo na makusanyo yanayopokelewa kutokana huduma nyinginezo chini ya Sheria hii;
- (e) zawadi, misaada na michango chini ya Sheria hii;
- (f) mkopo kutoka Serikalini, kwa mtu au taasisi yeyote;
- (g) mapato yatokanayo na mauzo ya mali au vyanzo vingine vya mapato

vinavyoteambulika na Baraza; na  
(h) fedha nyingine zozote zilizokopwa, kupokelewa au zipo tayari kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Baraza.

(2) Ada na tozo zitaainishwa kwenye Kanuni.

Taarifa za fedha za mwaka

**22.**-(1) Baraza kila mwisho wa mwaka wa fedha litaandaa taarifa ya utekelezaji ya mwaka ya shughuli zilizofanyika katika mwaka wa fedha na kuwasilisha taarifa hiyo kwa Waziri.

(2) Baraza litahakikisha taarifa ya fedha ya mwaka imeandaliwa na kukaguliwa ndani ya kipindi cha miezi mitatu baada ya mwaka wa fedha.

(3) taarifa za fedha zitajumuisha-

- (a) taarifa ya utendaji;
- (b) taarifa ya utekelezaji wa kifedha;
- (c) taarifa ya mtiririko wa mapato na matumizi;
- (d) taarifa ya mabadiliko ya faida au hasara; na
- (e) maelezo ya ufafanuzi wa taarifa za fedha.

Uwasilishwaji wa taarifa ya fedha ya mwaka

**23.**-(1) Baraza litawasilisha kwa Waziri nakala za taarifa za hesabu zilizokaguliwa pamoja na taarifa iliyoandaliwa na Mkaguzi wa Hesabu miezi mitatu kila baada ya mwisho wa mwaka wa fedha.

(2) Baraza litaandaa na kuwasilisha kwa Waziri taarifa ya makadirio ya mapato na matumizi ya Baraza kwa mwaka wa fedha unaofuata kwa ajili ya kuidhinishwa.

(3) Hakuna matumizi yatakayofanyika kutoka kwenye fedha za Baraza isipokuwa kwa idhini ya Baraza ndani ya makadirio ya mwaka wa fedha ambao matumizi hayo yatafanyika.

Usimamizi na

**24.**-(1) Baraza litatunza vitabu vya

udhibiti wa fedha

fedha na kuhifadhi kumbukumbu zake za uendeshaji kwa mujibu wa viwango vya kihisibu vya kitaifa.

(2) Baraza litawezesha upatikanaji na utuzwaji wa vitabu sahihi vya fedha na kumbukumbu zinazohusu-

- (a) mali na madeni;
- (b) stakabadhi za matumizi ya fedha na matumizi mengineyo ya fedha; na
- (c) taarifa ya hali ya fedha pamoja na taarifa inayoonyesha kiundani hali ya utendaji wa fedha katika kila mwaka wa fedha.

(3) Fedha na rasilimali za Baraza zitatumika kwa madhumuni yaliyowekwa na kusimamiwa kama ilivyoelekezwa chini ya Sheria hii.

(4) Matumizi ya fedha za Baraza yanatakiwa kufuatiliwa na kupitiwa.

Bajeti ya mwaka na bajeti ya nyongeza

**25.**-(1) Katika muda usiopungua mwezi mmoja, kabla ya kuanza kwa mwaka wa fedha Baraza litaidhinisha bajeti kwa kiasi cha fedha kinachotarajiwa kupokelewa na kutolewa katika mwaka huo wa fedha.

(2) Iwapo katika mwaka wowote wa fedha, Baraza linahitaji fedha ambayo haikutengwa au kiasi ambacho ni zaidi ya kiasi kilichotengwa kwenye bajeti ya mwaka huo, Baraza itaidhinisha bajeti ya nyongeza itakayoonesha mgawanyo huo.

(3) Bajeti ya mwaka na bajeti ya nyongeza zitakuwa kwa namna itakavyoainishwa na kuelekezwa na Waziri.

Misingi ya uendeshaji

**26.**-(1) Baraza-

- (a) litafungua na kuendesha vitabu vyote vya fedha, leja, jarida na vitabu vingine vya ziada vya fedha kulingana na miongozo ya kihisibu; na
- (b) litapitia na kubadili nyaraka ili

kuwezesha kujiendesha kibiashara iwapo itahitajika kufanya hivyo.

(2) Fedha zote zitakazopokelewa zitawekwa katika akaunti ya mapato na malipo yatafanyika katika akaunti ya matumizi.

(3) Hakuna matumizi yatakayotoka katika fedha za Baraza isipokuwa kama matumizi hayo ni sehemu ya mpango wa matumizi yaliyoidhinishwa na Waziri.

Mamlaka ya kuwekeza

**27.** Baraza linaweza, baada ya kupata ridhaa ya Waziri na kushauriana na Waziri mwenye dhamana na fedha, kuwekeza kiasi chochote cha fedha ambacho hakihitajiki kwa matumizi kwa wakati huo.

## SEHEMU YA TANO MASHARTI YANAYOHUSU NIDHAMU

Upokeaji wa malalamiko kwa Msajili

**28.**-(1) Endapo patakuwa na tuhuma kwamba mkemia, fundi sanifu kemia au fundi sanifu kemia msaidizi hawezi kuendelea kutekeleza majukumu ya taaluma hiyo, yatawasilishwa kwa Msajili ambaye baada ya kupokea atayawasilisha kwa Baraza.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, Mkemia, fundi sanifu kemia au fundi sanifu kemia msaidizi hatachukuliwa kuwa hafai kutekeleza majukumu ya taaluma hiyo endapoa-

- (a) ametenda kosa kinyume na maadili ya taaluma;
- (b) umahiri wake katika kazi unatiliwashaka;
- (c) ametiwa hatiani kwa kosa lolote chini ya Sheria hii au sheria nyingine yoyote;
- (d) ametiwa hatiani kwa kosa la kutokuwa mwaminifu, udanganyifu au makosa yoyote yanayohusu kukosa uadilifu;
- (e) anatumamiwa kuwa ametenda kosa lolote kinyume na mwenendo wa taaluma, uzembe au kukiuka

maelekezo yaliyotolewa chini ya Sheria hii;

- (f) ana udhaifu wa kiakili na imethibitishwa hivyo na bodi ya madaktari Tanzania au mamlaka ya uchunguzi wa kiafya ya nje ya nchi.

(3) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (2), neno “kinyume na maadili ya taaluma” litafasiriwa, kwa kufanya yafuatayo-

- (a) kuvunja masharti yaliyo chini ya Sheria hii au kanuni;
- (b) kusindwa kufuata vigezo, matakwa na mazuio ya usajili, kuandikishwa au kuoredheshwa kama mkemia, fundi sanifu kemia au fundi sanifu kemia msaidizi.
- (c) kuwa na mwingiliano wa kimasilahi ambayo yataleta athari kwa mteja na mkemia, fundi sanifu kemia au fundi sanifu kemia msaidizi;
- (d) kufanya kazi ya kitaaluma bila kuwa na cheti halali cha usajili, kuandikishwa, kuorodheshwa au cheti cha muda;
- (e) kujaribu kutumia cheti, namba au muhuri wa moto wa mwanataaluma mwingine au kujifanya ni mkemia, fundi sanifu kemia au fundi sanifu kemia msaidizi;
- (f) kusaidia kufanya kazi ya taaluma ya kemia kinyume na taratibu na mtu yeyote;
- (g) kutoa taarifa au nyaraka za udanganyifu kwenye Baraza kwa ajili kupata cheti cha usajili, kuandikishwa au kuorodheshwa; au
- (h) kujifanya kuwa mwanataaluma ya kemia aliyesajiliwa, kuandikishwa na kuorodheshwa au kuwa na cheti cha muda.

(4) Malalamiko yoyote chini ya kifungu hiki yataambatishwa na tamko la kisheria

liliofanywa na mlalamikaji au mtu yeyote anayemwakilisha mlalamikaji au mtu yeyote mwenye maslahi katika tendo lililosababisha malalamiko hayo.

(5) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (4) Baraza, kwa ridhaa yake, litaamua kuanzisha uchunguzi wowote wa awali kwa mkemia, fundi sanifu kemia au fundi sanifu kemia msaidizi; iwapo litaridhika na taarifa zilizopokelewa kama zinatoshleza kufanya uchunguzi.

(6) Isipokuwa kwa malalamiko yaliyofanywa chini ya kifungu kidogo cha (2), hakuna uchunguzi utakaoendelea mpaka tamko la kisheria limepatikana.

Kusimamishwa  
kwa muda  
kupisha  
uchunguzi

- 29.** Baraza linaweza baada ya kupokea-
- (a) malalamiko dhidi ya mwanataaluma waya kemia; au
  - (b) ripoti kutoka kwa mamlaka ya usimamizi,

kumsimamisha kutekeleza majukumu ya kikemia kwa muda mwanataaluma yeyote wa kemia wakati anasubibili uchunguzi kukamilika.

Taratibu za  
uchunguzi

**30.**-(1) Iwapo Baraza kwa maoni yake litaona kwamba kuna kesi ya kujibu, litaekeleza kufanyika kwa uchunguzi.

(2) Baraza litatoa fursa kwa mwanataaluma ya kemia anayetuhumiwa dhidi ya ukiukaji wa maadili, kufika mbele ya Baraza kwa ajili ya kusilizwa na anaweza kuwakilishwa na wakili.

(3) Iwapo mwanataaluma wa kemia atashindwa kufika kwenye uchunguzi pasipo sababu maalum na endapo Baraza litaridhiku kuwa taarifa ilimfikia mwanataaluma huyo Baraza laweza kuendelea na uchunguzi kama vile mwanataaluma angekuwepo.

Mamlaka ya  
nidhamu ya

**31.**-(1) Baraza baada ya kufanya uchunguzi wa kina chini ya masharti ya Sheria

Baraza

hii linaweza-

- (a) kutoa amri ya kuondoa jina la mwanataaluma ya kemia kwenye Rejesta;
- (b) kutoa amri ya kusimamishwa kufanya kazi ya mwanataaluma ya kemia kwa kipindi kitakachoonekana kinafaa;
- (c) kutoa tahadhari au onyo kwa mwanataaluma ya kemia, au
- (d) kutoza faini au kuamuru kulipwa kwa gharama zilizotumika katika uchunguzi au gharama nyingine, kama itakavyokuwa.

(2) Msajili, ndani ya siku saba baada ya uchunguzi kukamilika, atawasilisha maamuzi ya Baraza kwa pande zote zinazohusika.

Mamlaka ya kumuita shahidi

**32.** Baraza litakuwa na mamlaka ya kumuita shahidi yeyote muhimu na kumtaka kuwasilisha nyaraka kwa lengo la uchunguzi uliofanyika chini ya Sheria hii.

Kushindwa kuhudhuria uchunguzi

**33.**-(1) Mtu ambaye amepewa wito wa kuhudhuria na kutoa ushahidi au nyaraka yoyote kwa ajili ya uchunguzi wowote uliofanyika chini ya kifungu cha 32-

- (a) atashindwa bila sababu maalumu kutii wito;
- (b) atashindwa kutoa nyaraka itakayohitajika;
- (c) atakataa bila sababu maalumu kujiibu maswali atakayoulizwa na Baraza; au
- (d) kwa makusudi kuingilia mwenendo wa mashauri ya Baraza au kumtukana mjumbe wa Baraza,

anatenda kosa.

(2) Mtu yeyote atakayetoa ushahidi mbele ya Baraza, kuhusiana na ushahidi uliotolewa naye au nyaraka yoyote aliyoitoa, atakuwa na haki na wadhifa kama shahidi mbele ya mahakama.



Rufaa

**34.**-(1) Mtu yeyote ambaye hataridhishwa na maamuzi ya Baraza, anaweza kukata rufaa kwa Waziri ndani ya kipindi cha miezi mitatu kutoka tarehe ya kupewa taarifa ya maamuzi ya Baraza dhidi yake.

(2) Waziri, ndani ya siku thelathini tangu kupokea rufaa, ataamua rufaa hiyo.

(3) Waziri anaweza kubatilisha, au kuruhusu rufaa yoyote au kubadilisha maamuzi ya Baraza au kutoa maelekezo mengine kadri itakavyokuwa lazima.

(4) Waziri baada ya kutoa uamuzi wa rufaa, atampatia mrufani, ndani ya mwezi mmoja, nakala ya maamuzi hayo.

**SEHEMU YA SITA  
MASHARTI JUMLA**

Kanuni

**35.**-(1) Waziri kwa kushauriana na Baraza atatengeneza kanuni za utekelezaji wa malengo na madhumuni ya Sheria hii.

(2) Bila kuathiri masharti ya jumla ya kifungu kidogo cha (1), Waziri anaweza kutengeneza kanuni za kufafanua juu ya-

(a) namna, aina ya fomu na mwenendo wa maombi ya usajili, uorodheshwaji, uandikishwaji au ubakishwaji na ufutwaji kwenye Rejesta;

(b) uteuzi, mamlaka na sifa za wakaguzi na jinsi ya kufanya ukaguzi kwa madhumuni ya Sheria hii;

(c) tozo na gharama nyingine;

(d) kuhifadhi, kuwekeza na kutumia fedha na mali za Baraza; na

(e) taratibu za Baraza kufanya uchunguzi, kuita mashahidi na kutoa ushahidi katika uchunguzi, pamoja na mamlaka ya kuchukua ushahidi chini ya kiapo.

Taratibu

**36.**-(1) Baraza litaweka, kwa kuthibitishwa na Waziri, taratibu za utekelezaji wa madhumuni na masuala mengine yanayohitajika chini ya Sheria hii.

(2) Bila kuathiri mamlaka yaliyotajwa chini ya kifungu hiki kwa ujumla wake, Baraza linaweza kuweka taratibu za-

- (a) kuainisha sifa zitakazotambulika kwa mtu mwenye hadhi ya kusajiliwa, kuorodheshwa na kuandikishwa chini ya Sheria hii;
- (b) kuainisha maadili na viwango vya utendaji vya wanataaluma ya kemia; na
- (c) masuala mengineyo ambayo ni muhimu katika utekelezaji wa Sheria hii.

Makosa na adhabu

**37.**-(1) Mtu yeyote ambaye atatenda kosa kinyume na masharti ya Sheria au Kanuni za Sheria hii ambapo adhabu haijaainishwa atawajibika kulipa faini isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja.

(2) Mtu yeyote aliyesajiliwa, kuorodheshwa au kuandikishwa chini ya Sheria hii hatajihusha na kazi zilizo kinyume cha Sheria au kushirikiana na mtu anayefanya kazi za aina hiyo.

(3) Mtu hatajipatia au kujaribu kujipatia usajili au kuorodheshwa au kuandikishwa kwa njia ya udanganyifu au chini ya tamko la uongo, hati, maombi au uwasilishaji, iwapo kwa maandishi au matamshi au kwa makusudi anafanya au kusababisha udanganifu kufanyika ndani ya Rejesta.

(4) Mtu yeyote ambaye atakiuka masharti ya kifungu kidogo cha (2) na (3) anatenda kosa na atawajibika, iwapo atatiwa hatiani, kulipa faini isiyopungua shilingi laki tano na kutumikia kifungo kwa kipindi cha miaka miwili, au yote.

Kutangaza  
majina ya  
wanataaluma  
wa kemia

**38.** Waziri, kwa amri itakayochapishwa kwenye *Gazeti* la Serikali, atatangaza majina ya Wanataaluma wa kemia.

Kinga kwa  
makosa

**39.** Bila kujali suala alilotenda, Mkemia Mkuu wa Serikali, mjumbe yeyote wa Bodi, mjumbe wa kamati, mwajiliwa au mtu yeyote aliyepewa mamlaka ya kutekeleza majukumu chini ya Sheria hii, hatahesabiwa kuwa na hatia endapo ametenda kosa akiwa katika hatua za utekelezaji wa majukumu yake kwa nia njema kulingana na sheria, kanuni au sheria ndogondogo zilizotungwa chini ya Sheria hii.

Ufililishaji wa  
makosa

**40.**-(1) Baraza linaweza, iwapo litadhirika kwamba mtu ametenda kosa chini ya Sheria hii, kufililisha kosa hilo kwa kupokea kutoka kwa mtu huyo kiasi cha fedha ambacho hakitozidi shilingi milioni tano.

(2) Iwapo kosa limefifishwa kwa mujiibu wa kifungu kidogo cha (1) na shauri linaletwa dhidi ya mkosaji kwa kosa hilo hilo, itakuwa ni utetezi wa msingi kwa mkosaji kuitibitishia mahakama kwamba kosa ambalo anashtakiwa nalo limeshafifishwa chini ya kifungu kidogo cha (1).

(3) Mtu yeyote ambaye haridhishwi na amri yoyote iliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1), anaweza, ndani ya siku thelathini tangu tarehe ya amri hiyo, kukata rufaa kwa Waziri.

(4) Iwapo mtu yeyote anashindwa kutekeleza amri iliyotolewa chini ya kifungu hiki ndani ya muda ulioanishwa, mbali na kiasi cha fedha kilichoamriwa, Baraza litamuamuru mhusika kulipa riba kwa kiwango kilichoainishwa kwenye kanuni.

(5) Waziri atatengeneza kanuni zinazoainisha makosa yatakayofifishwa na utaratibu wa kufifisha makosa chini ya sheria hii.

**JEDWALI**

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 4)*

---

**UTEUZI, MUUNDO NA MWENENDO WA BARAZA**

- Mwenyekiti                    **1.**-(1) Mwenyekiti anatakiwa awe mwelewa, mwa-minifu na mwenye maadili ambaye ana uzoefu kwenye masuala ya kemia.  
(2) Wajumbe watamchagua kutoka miongoni mwao mjumbe mmoja atakayekuwa Makamu wa Mwenyekiti.
- Muda wa kukaa madarakani                    **2.**-(1) Mwenyekiti na wajumbe watahika nyazifa zao kwa kipindi cha miaka mitatu na watakuwa na sifa za kuteuliwa tena kwa kipindi kingine kimoja, isipokuwa pale uteuzi wao utakapokuwa umesitishwa na Waziri, au ujumbe wao utakuwa umesitishwa kwa sababu zozote zile.  
(2) Kwa mjumbe ambaye ameteuliwa kutokana na kushika madaraka katika ofisi yake, atakoma kuwa mjumbe mara atakapoacha kushika madaraka katika ofisi hiyo.  
(3) Mjumbe atakoma kuwa mjumbe kama-  
(a) atafariki au kujiuzuru kwa sababu zozote zile;  
(b) atashindwa kuhudhuria vikao vitatu vya Baraza mfululizo bila sababu za msingi;  
(c) amehukumiwa kwa makosa ya jinai kwa zaidi ya miezi sita;  
(d) atapata ugonjwa wa akili; au  
(e) Atazuiliwa kufanya kazi kwa mujibu wa Sheria hii.  
(4) Pale mjumbe aliyeteuliwa atakoma kuwa mjumbe kwa sababu zilizoainishwa kwenye kifungu kidogo cha (3), Waziri atateua mtu mwingine kuziba nafasi yake na mtu aliyeteuliwa atakuwa mjumbe kwa kipindi kilichobakia cha mjumbe wa awali mtangulizi wake.  
(5) Iwapo mjumbe wa Baraza ni mjumbe kutokana na ofisi anayoshika hataweza kuhudhuria kikao chochote cha Baraza kwa sababu yoyote ile, anaweza kuteua mtu mwingine kutoka katika shirika lake kuhudhuria kikao kwa niaba yake katika nafasi yake.
- Vikao vya Baraza                    **3.**-(1) Baraza litakuwa na vikao katika hali ya kawaida angalau kimoja kila baada ya miezi mitatu katika muda na sehemu kadiri itakavyoonekana inafaa ili kuendesha shughuli zake.  
(2) Bila kujali kifungu cha (1), Mwenyekiti anaweza, baada ya kupata idhini ya theluthi mbili ya wajumbe kuitisha kikao cha dharura kujadili suala linalohitaji uamuzi wa haraka.

(3) Mwenyekiti, au endapo hayupo, Makamu Mwenyekiti anaweza wakati wowote kuitisha kikao cha dharura baada ya kupokea maombi ya maandishi kutoka kwa wajumbe walio wengi.

(4) Pale Mwenyekiti anapokuwa hayupo, vikao vitaongozwa na Vikao vitaongozwa na Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti na pale ambapo wote hawapo, wajumbe watakaokuwepo kwenye kikao, watachagua mmoja wa wajumbe kuwa kuongoza kiakao.

Akidi

**4.**-(1) Akidi ya katika kikao ya chochote cha Baraza litakuwa ni theluthi mbili ya wajumbe.

(2) Mambo ya mapendekezo katika kikao cha Baraza, yataamuliwa na idadi kubwa ya kura za wajumbe waliohudhuria.

(3) Uhalali wa taarifa yoyote ya kikao cha Baraza iliyoundwa kihalali hautaathiriwa na kukosekana kwa mjumbe yeyote asiyehudhuria au kwa kasoro itakayotolewa na mjumbe asihudhuria kikao.

Maelekezo  
ya Baraza

**5.**-(1) Maagizo, maelekezo, matangazo au hati iliyotayarishwa au kutolewa kwa niaba ya Bodi inatakiwa kutiwa saina na-

(a) Mwenyekiti; au

(b) katibu au afisa yeyoye aliyeidhinishwa kwa maandishi kwa niaba yake.

Mhuri

**6.** Mhuri wa Baraza hautawekwa kwenye waraka wowote isipokuwa tu mbele ya Msajili au afisa mwingine wa Baraza atakayeteuliwa na Msajili.

Mienendo ya  
mikutano

**7.** Kwa kuzingatia masharti ya Jedwali hili, Baraza litasimamia mienendo ya mikutano.

---

**MADHUMUNI NA SABABU**

---

Madhumuni ya Muswada huu, ni kutunga Sheria ya Usimamizi wa wakemia, mafundi sanifu kemia na mafundi sanifu kemia wasaidizi. Muswada huu unapendekeza kutungwa kwa Sheria ya Baraza la Wanataaluma ya Kemia na unaainisha majukumu, usimamizi na udhibiti wa wanataaluma ya kemia. Inapendekezwa kuweka utaratibu wa kishekria kwa ajili ya kusimamia wanataaluma ya kemia katika sekta binafsi na umma kwa kuzingatia sifa na vigezo vya usajili.

Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Kuu Sita.

Sehemu ya Kwanza inahusu masuala ya awali ikihusisha tafsiri ya Sheria, tarehe ya kuanza kutumika na wigo wa matumizi ya Sheria hii.

Sehemu ya Pili inahusu uanzishwaji wa Baraza la Kusimamia Wanataaluma ya Kemia, kamati na majukumu yake. Sehemu hii pia inaainisha majukumu ya Baraza ambayo ni pamoja na kuwa mamlaka mahususi ya kusajili wakemia, kuorodhesha fundi sanifu kemia na kuandikisha fundi sanifu kemia wasaidizi wa kemia. Aidha, Sehemu hii pia inabainisha mamlaka ya Baraza, uteuzi na majukumu ya Msajili, ambapo majukumu ya Msajili ni pamoja na kutoa vyeti vya usajili, kutunza rejesta, taarifa za akaunti na kumbukumbu nyinginezo zinazohusu fedha na rasilimali.

Sehemu ya Tatu inaainisha masharti yanayohusu usajili, uandikishwaji na uorodheshwaji wakemia, mafundi sanifu kemia na mafundi sanifu kemia wasaidizi Tanzania. Sehemu hii pia inabainisha sifa za kusajiliwa, kuorodheshwa na kuandikishwa, kwa utaratibu huo. Vifungu vinavyohusu mafunzo kwa vitendo, usajili wa muda, usitishaji, ubatilishaji au ufutaji wa cheti vimebainishwa katika sehemu hii pia.

Sehemu ya Nne inahusu vyanzo vya mapato ya Baraza na inatoa mamlaka kwa Baraza kuwekeza fedha ili kuendeleza wanataaluma ya kemia.

Sehemu ya Tano inabainisha vifungu vinavyohusu masharti ya nidhamu, upokeaji na ushughulikiaji wa malalamiko dhidi ya mkemia, fundi sanifu kemia au fundi sanifu kemia msaidizi. Sehemu hii pia inabainisha vifungu kuhusu uchunguzi wa Baraza juu ya matendo ya mwanataaluma ya kemia endapo ametuhumiwa kukiuka maadili ya wanataaluma ya kemia. Sehemu hii pia inabainisha vifungu vinavyohusu mam-laka ya nidhamu ya Baraza na taratibu za kukata rufaa.

Sehemu ya Sita inabainisha masharti ya jumla, kwa kuainisha vifungu vinavyohusu makosa na adhabu, utoaji wa taarifa na usababishaji wa hasara. Aidha, Sehemu hii inapendekeza kumpa Waziri uwezo wa kutengeneza kanuni za utekelezaji wa malengo na madhumuni ya Sheria inayopendekezwa kutungwa. Sehemu hii pia inampa Waziri uwezo wa kufanya mabadiliko ya kanuni na majedwali yaliyopendekezwa katika Sheria hii inapobidi.

Dar es Salaam,  
10 Mei, 2016

**UMMY A. MWALIMU**  
*Waziri wa Afya, Maendeleo ya  
Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto*